

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI
MTIHANI WA UALIMU DALAJA A**

638

VIELELEZO NA TEKNOLOJIA

Muda: Saa 3

Jumatatu, 14 Mei 2012 asubuhi

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A na B.
2. Jibu maswali **yote** kutoka katika sehemu A na maswali **manne(4)** kutoka katika sehemu B.
3. Soma kwa makini maelekezo ya kila sehemu na ya kila swalii.
4. Majibu yote yaandikwe kwa kalamu ya wino wa bluu au mweusi isipokuwa michoro ambayo itachorwa kwa penseli.
5. Vikokotozi **haviruhusiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
6. Simu za mkononi **haziruhusiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
7. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. (a) Projekta ni nini?
(b) Toa faida tatu za kutumia projekta kama kifaa cha kufundishia na kujifunzia.
2. (a) Eleza maana ya mali ghafî kama linavyotumika katika somo la Vielelezo na Teknolojia.
(b) Toa sababu tatu kuainisha umuhimu wa mali ghafî katika kubuni na kufaragua zana za kufundishia na kujifunzia.
3. Fafanua matumizi manne ya medali katika kufundishia na kujifunzia.
4. Eleza hatua nne zinazotakiwa kufuatwa wakati wa kutumia filamu kama zana ya kufundishia na kujifunzia.
5. (a) Eleza kwa ufupi madhumuni ya kutumia chati wakati wa kufundisha na kujifunza.
(b) Pendekeza namna tatu ambavyo chati zinaweza kutunzwa.
6. Bainisha aina nne ya vielelezo na teknolojia kisasa na eleza kwa kifupi matumizi yake katika mchakato wa kufundisha na kujifunza.
7. Bainisha sifa nne zinazoweza kutumika kutathmini ubora wa zana za kufundishia na kujifunzia.
8. Fafanua kwa mifano namna ambavyo zana zifuatazo zinaweza kutumika kufundisha somo la Vielelezo na Teknolojia.
(a) Vielelezo na Teknolojia Masikizi (c) Malengo ya jumla
(b) Malengo mahsus (d) Vielelezo na Teknolojia Maono-Masikizi.
9. Toa sababu nne zinazoyafanya machapisho kuwa ni vielelezo vinavyotumiwa zaidi na walimu na wanafunzi katika kufundishia na kujifunzia.
10. Bainisha changamoto nne zinazoweza kujitokeza wakati mwalimu anapotumia Kompyuta kama chanzo cha taarifa.

SEHEMU B (Alama 60)

Jibu maswali **manne (4)** kutoka sehemu hii.

11. Tathmini umuhimu wa maandishi ya rejea katika kutayarisha somo.
12. Kwa kutumia mifano katika mazingira ya Tanzania, fafanua aina ya zana ambazo mwalimu anaweza kutumia katika darasa jumuishi lenye wanafunzi wasioona.

13. Eleza faida tano za matumizi ya zana za kufundishia wakati wa kufundisha na kujifunza.
14. 'Picha huwakilisha zaidi ya maneno elfu moja' Jadili usemi huu katika muktadha wa matumizi ya vielelezo na teknolojia.
15. Kwa kutumia mifano, chambua changamoto zinazoweza kujitokeza Televisheni inapotumika kama zana ya kufundishia.
16. Fafanua mambo matano ambayo mwalimu anatakiwa kuyazingatia wakati wa kubuni na kufaragua zana za kufundishia na kujifunzia.
17. Eleza faida tatu na hasara mbili za kutumia intaneti kama chanzo cha taarifa za kufundishia na kujifunzia. Toa mifano kuthibitisha hoja zako.
18. Fafanua manufaa matano ya kutumia vielelezo na teknolojia maono katika ufundishaji na ujifunzaji.